TANGAZO LA SERIKALI NA. 599 la tarehe 19/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu 22(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI KARUGAMBA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi Karugamba ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la hifadhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi Karugamba.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA BUHIGWE

MSITU WA HIFADHI KARUGAMBA


*Makadirio ya Eneo:* Hekta 55.42 au Kilometa za Mraba 0.55

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Karugamba linalopatikana Wilaya ya Buhigwe, Mkoa wa Kigoma kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2763 ya mwaka 2018 (Skeli 1:10,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 599 (linaendelea)*

**KARUGAMBA FOREST RESERVE**
**BUHIGWE DISTRICT**
**AREA 55.42Ha OR 0.55SQ KILOMETRES**




Dodoma,
___24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI
*Waziri wa Maliasili na Utalii*